



### Maswali

1. Mbona Mungu alichagua mfalme mpya?
2. Mungu aliambia Samweli aende wapi?
3. Mungu alimwambia Samweli afanye nini kwa kisiri?
4. Mungu alikuwa amechagua mwana wa nani kuwa mfalme mpya?
5. Mzaliwa wa kwanza wa Yese alikuwa nani?
6. Samweli alifikiria nini alipoona Eliabu?
7. Mungu aliambia Samweli nini?
8. Mwana yupi wa Yese alipagwa mafuta na Samweli awe mfalme?
9. Mbona Sauli alihuzunika?
10. Daudi alifanya nini kuchangamsha Sauli?

### Majibu

1. Mungu alichagua mfalme mpya kwa sababu Sauli alimuasi.
2. Mungu alimwambia Samweli aende Bethlehemu.
3. Mungu alimwambia Samweli apage mfalme mpya mafuta atawale Israeli.
4. Mungu alikuwa amechagua mwana mmoja wa Yese kuwa mfalme mpya.
5. Eliabu alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Yese.
6. Eliabu alikuwa wa nguvu na sura nzuri. Samweli alifikiria Mungu alikuwa amemchagua.
7. Mungu haangalii zura ya nje vile mtu anaonekana. Mungu huangalia moyo.
8. Mwana wa mwisho wa Yese alipagwa mafuta na Samweli kuwa mfalme.
9. Sauli alikasirika kwa sababu Mungu hakuwa karibu naye.
10. Daudi alipiga kinubi ili amchangamshe Sauli.

# 59 Daudi anapakwa mafuta ya kifalme

### Kwa Biblia

1 Samweli mlango wa 16

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huangalia moyo na tabia. Mungu hangalii sura. Mungu anataka tumpende na kumtii

### Somo

Tumekuwa tukijifunza juu ya Sauli. Alikuwa mfalme wa Israeli wa kwanza. Lakini Sauli hakupenda Mungu wala kumtii. Sauli aliasi Mungu, kwa hivyo Mungu akachagua mfalme mpya. Sauli alikubaliwa kutawala kwa muda wote aliokuwa hai. Lakini Mungu alisema wana wake hawakutawala baada yake. Mungu alichagua mtu aliyekuwa na tabia mzuri ili atawale Waisraeli na kuwafundisha juu ya Mungu.

Siku moja Mungu aliambia Samweli aende Bethlehemu. Aliambia Samweli aende atolee dhabihu kule. Mungu akamwambia kwamba, wakati atakuwa akitoa dhabihu apake mfalme mpya wa Israeli mafuta. Yule mfalme mpya atakuwa mmoja wa wana wa mtu aitwae Yese. Mungu ataonyesha Samweli ni mwana yupi wa Yese amechaguliwa kuwa mfalme.

Samweli alienda Bethlehemu. Alienda kwa nyumba ya Yese. Samweli aliambia Yese kwamba Mungu amechagua mmoja wa wana wake kuwa mfalme mpya wa Israeli. Yese aliita wana wake saba wasimame mbele ya Samweli.

Samweli aliangalia Eliabu. Yeye ndiye alikuwa mzaliwa wa kwanza. Eliabu alikuwa mrefu na wa sura nzuri. Alikuwa mwenye nguvu. Samweli alifikiri kwamba huyo ndiye Mungu amemchagua kuwa mfalme. Lakini Mungu hakukuwa amechagua Eliabu kuwa mfalme.

Mungu aliambia Samweli, “Usiangalia sura yake wala kimo cha urefu wake. Mungu hangalii maumbile ya mtu ama kama ana nguvu au la. Watu hutaka mtu awe mrefu au na sura nzuri au wa nguvu. Lakini Mungu hana haja na vitu hivyo. Mungu huutazama moyo.” Mungu alikuwa amechagua mtu wa hekima na atakaye tawala watu wake vizuri.



Wana wa Yese wawili walikuja na kusimama mbele ya Samweli. Lakini Mungu hakuwa amewachagua. Wana wanne wa Yese wengine walikuja mbele ya Samweli mmoja baada ya mwingine. Bado Mungu hakukuwa amewachagua.



Samweli aliambia Yese, “Mungu hajachagua yeyote kwa hao wana saba. Kuna mwana mwingine.” Yese alimwambia kuna mwana wake wa mwisho na ni kijana mdogo. Alikuwa nje vilimani anachunga kondoo. Samweli alimwambia amlete yule mwanawe wa mwisho.

Yese alimleta huyo mwanawe wa mwisho kutoka kwa vilima. Jina lake ni Daudi. Daudi aliletwa na kusimama mbele ya Samweli. Daudi alikuwa kijana mdogo. Alikuwa wa ngozi ya weupe iliyobadilishwa kwa jua na alionekana vizuri. Samweli alisema, “Huyu

ndiye mtu Mungu amemchagua kuwa mfalme wa Israeli.” Samweli alimpaka mafuta awe mfalme.

Sauli aliendelea kutawala kama mfalme wakati wote alipokuwa hai. Wakati wa Daudi kutawala ulikuwa bado. Lakini Mungu alikuwa amemchagua kama mfalme mpya. Daudi alirudi kwenda kuchunga kondoo. Kuanzia hapo Mungu alikuwa na Daudi. Daudi alipenda Mungu na kuwa karibu naye. Daudi alikuwa mchungaji. Alijifunza kuwa mvumilivu. Alijifunza kuwa mchungaji wa kondoo. Daudi alipenda muziki na nyimbo. Alikuwa akipiga kinubi wakati alichunga kondoo. Aliandika zaburi au nyimbo nyingi za kumtukua Mungu. Tunaweza kusoma nyimbo nyingi za Daudi kwa kitabu cha Zaburi katika Biblia. Wimbo wa Daudi unaojulikana sana ni Zaburi 23.

Mungu alikataa Sauli kwa sababu hakutii amri za Mungu. Mungu hakukuwa na Sauli. Sauli alijua kwamba Mungu hakukuwa karibu naye. Sauli alihuzunika sana. Wafanyikazi wa Sauli walimshauri a imbiwe nyimbo labda ingemchangamsha. Walimwambia juu ya kijana mchungaji aliyekuwa mwerevu wa kucheza kinubi. Huyo mchungaji kijana alikuwa Daudi.



Wafanyikazi wa Sauli waliambia Daudi aje achezee mfalme Sauli kinubi. Wakati wowote Sauli alipokuwa na huzuni, Daudi alimchezea kinubi ili achangamke.

Sauli alipenda Daudi. Alimfanya awe wa kumbebea silaha.

Kwa namna hii, Mungu alileta mfalme wa kale na mfalme mpya pamoja! Wakati huu Sauli hakujua kwamba Daudi alikuwa amepagwa mafuta ya kuwa mfalme mpya. Baadaye alipojua, alighadhabika sana na kuwa na wivu.